# Kisima chenye Hekima

## na Hadithi Nyingine



Wahariri

Fred, C. N. W. Simiyu na Leonard Sanja Leo

# Kisima chenye Hekima

# na

# Hadithi Nyingine

## Wahariri

Fred, C. N. W. Simiyu & Leonard Sanja Leo

**Mradi wa CHAKITA 2026**

Kimepokewa zawadi kwa
Maktaba ya Chuo Kikuu cha
Kibabii (Kona ya Ken Walibora)
ya Mwandishi 01/07/2026

TUNU PUBLISHERS

# Dibaji

Mkusanyiko huu ni wa kipekee maanake ni wa kwanza kufanywa na chama cha kitaaluma cha CHAKITA. Hivyo basi, ni kazi ambayo inagusa kina cha roho za wapenzi wote wa lugha hii adhimu ambao ni wanachama. Diwani hii ni ya kwanza katika mchakato mkubwa unaotarajiwa. Kufikia sasa, uandishi wa hadithi fupi umepevuka sana nchini Kenya na kwa wakati huu unashindana na riwaya na kuupiku uandishi wa tamthilia ambao ni haba. Siyo kwamba tamthilia haziandikwi, la! Zipo tu ingawa hazichapishwi kwa wingi. Muhimu zaidi ni kuhusu toni mbalimbali ambazo tunazishuhudia katika utunzi wa hadithi fupi. Baadhi ya toni hizi ni kero, usisimuzi wa fitina, uchochezi wa hatua mwafaka na hata huzuni. Toni hizi zimetumiwa kuibua masuala mtambuko katika jamii. Pia ikumbukwe kwamba, kipengele hiki cha kimtindo kimechangamkiwa sana na waandishi wa hadithi fupi hivi karibuni.

**Dkt. Fred. C. N. W. Simiyu - Chuo Kikuu cha Kibabii & Chuo Kikuu cha *the Free State*; na Leo Sanja Leonard - Chuo Kikuu cha Nairobi.**

**Machi 2026.**

Utanzu wa hadithi fupi unatofautiana na riwaya kutokana na sifa wa urefu. Sifa hii ndiyo inayosababisha ukunjufu wa kifani katika [illegible] na usahili wayo katika hadithi fupi. Katika masuala ya fani, mwandishi wa riwaya huwekewa mipaka na ubunifu wake ilhali katika hadithi fupi mwandishi hudhibitiwa na mawanda yake mafupi na hulazimika kueleza mambo kwa muhtasari. Suala la urefu pia husababisha hadithi fupi kuwa na mianzo maalum na vimalizio maalum. Hii ni kwa sababu, mwandishi hana uhuru mkubwa wa kujieleza kama katika riwaya. Hadithi fupi ya Kiswahili pia ina uhusiano na ngano za fasihi simulizi. Tanzu zote ni fupi. Ngano zililenga kufunza na kwa hivyo ziliandikwa kwa njia maalum. Ngano pia zina mianzo maalum ambayo kuhusu kipindi cha zamani ambacho hakielezwi waziwazi. Hata hivyo, hadithi fupi hazina mianzo maalum na hulenga kipindi mahsusi cha wakati.

Ngano hutambulika sana kwa matumizi ya wahusika wa kiajabu ambao uwezo wao huzidi ule wa binadamu wa kawaida. Ingawaje kigezo hiki kimetumiwa na baadhi ya wahakiki kutofautisha tanzu hizi mbili ni muhimu kutambua mtagusano uliopo baina ya tanzu hizi mbili unaowaruhusu waandishi wa hadithi fupi pia kutumia wahusika wa sampuli hii ili kutimiza malengo yao. Ohly (1977) amechunguza baadhi ya vijitanzu ambavyo vinakaribiana na utanzu wa hadithi fupi. Katika makala yake *Problems of Literary Genres in Kiswahili* anamulika vijitanzu kadhaa ambavyo vinakaribiana [illegible] na utanzu wa hadithi fupi kama vile; hadithi, hekaya, ngano, [illegible] na masimulizi. Vijitanzu alivyovitaja ni vitangulizi muhimu wa hadithi fupi ya Kiswahili lakini ni wazi kwamba baada ya [illegible] utanzu wa hadithi fupi msingi vilianza kutokomea. Ni muhimu pia kutambua ya kwamba, uhusiano na Fasihi Simulizi umesababisha athari muhimu katika hadithi fupi za kisasa. Athari [illegible] huonekana katika wahusika waliokiuka uwezo wa binadamu.

Kimapisi, utanzu wa hadithi fupi katika fasihi ya Kiswahili uliwezeshwa mwanzoni na magazeti ambayo zilichapishwa ndani (Wamitila 2003). Hadithi fupi ya Kiswahili ina historia ndefu.

muhimu za kuzingatia hilo katika mfumo wa elimu na usomi kwa ujumla. Hadithi yake Nandama yenye anwani ya *Mtu Mtandaoni* inashadidia ukweli kwamba, mui huwa mwema. Hii ni kwa sababu mhusika mkuu anabadilika na kutumia mitandao ya kijamii vizuri na hata kufanikiwa maishani. Iribe anauliza swali nyeti, ambalo ni mwana wa kiume ni wa nani katika kisa cha *Mwangwi wa Kilio*. Aidha, Mutenyo anataka hatua zichukuliwe dhidi ya wanaouza mihadarati na pia wazazi wawajibike kwa kuwashauri wana wao badala ya kuachia watu wengine na asasi kama shule katika hadithi ya *Baba wa Langoni*. Isitoshe, Luteshi katika hadithi ya *Sitaki Mume* anaangazia mahusiano ya kiholela miongoni mwa vijana na madhara yake huku akitoa rai kuwa, vijana wenyewe pia wanastahili kuchangamkia maadili na bidii kazini. Zaidi ya hayo, Sanja ndani ya hadithi ya Ndoto za *Pacha na Pachika* anapambanua namna watu wa ughaibuni wanavyodhulumu Waafrika na hasa vijana wenye vipawa kama wanariadha bila wasimamizi wao kuwajibika wala kupinga dhuluma hizo.

Halikadhalika, hadithi ya *Nizike Mtandaoni* yake Simiyu na ya Mwalwa yenye anwani *Mchuuzi* ni visa ambavyo vinataka jamii kuchangamkia suala la malezi, elimu na kujirudi. Hadithi hizi pia zinajumuisha madhara ya teknolojia na mitandao ya kijamii. Fauka ya hayo, hadithi ya *Mke wa Mama* iliyotungwa na Rayya inaonyesha umuhimu wa uhuru wa vijana kufanya maamuzi muhimu, pamoja na kupambanua nafasi ya udini katika kudhibiti watoto. Halikadhalika, Wamitila katika hadithi ya kichwa *Tandabui la Maisha* anatetea hadhi ya mtoto wa kiume katika jamii inayompendelea mtoto wa kike. Naye Mohochi katika hadithi ya *Kadhia za Maandamano* anahoji kwamba, ni muhimu kusikiliza sauti ya wananchi. Wanyonyi katika hadithi ya *Njiapanda* anamulika suala la utepetevu katika jamii ya kisasa hususan katika malezi kuanzia kwa mzazi, mwalimu na mwanafamilia. King'ei katika hadithi ya *Pendo la Mhisani* amepambanua athari za malezi na uuzaji watoto kwa wageni kwa sababu ya umaskini. Hadithi ya Funzo la Maisha yake Mbatia, inaibua

alivyojifunza kuhusu kupitia nyanya yake katika hadithi yake yenye anwani *Shule ya Nyanya*.

Mkusanyiko huu unaibua swali muhimu, je, jamii inastahili kufanya nini? Ni mkusanyiko unaoibua toni tulizotaja hapo awali na msomaji hana budi kusisimka, kunaswa na kuvutwa na uketo wa yaliyomo ambayo yana mchomo mkali wa kihisia, unaompa ilhamu ya kutaka kuchukua hatua kuhusiana na yaliyomo. Mkusanyiko huu umejumuisha waandishi wanaoinukia na wale ambao wamebobea. Muhimu hata hivyo ni kwamba, kuna uchu na ari ya kuibua masuala nyeti katika jamii na kuyaangazia kwa jicho pevu na kalamu yenye uzito wa usimulizi na mbinu faridi za kughani. Tunawashukuru walimu na wanafunzi waliosoma baadhi hadithi zilizomo na kutoa maoni yao ambayo yameondokea kuwa hazina kuu kwetu. Hii ni kazi inayolenga wanafunzi, wanachuo, wasomaji na wahakiki wa fasihi. Asanteni.

**Wahariri, Machi 2026.**

# Yaliyomo


Dibaji ........ iii

Utangulizi ........ iv

Tandabui la Maisha – K. W. Wamitila ........ 1

Baba wa Langoni – Aidah Mutenyo ........ 17

Kadhia za Maandamano – Ernest Sangai Mohochi ........ 32

Ndoto za Pacha na Pachika – Sanja Leo ........ 44

Sitaki Mume – Beatrice Luteshi ........ 58

Mwangwi wa Kilio – P. I. Iribemwangi ........ 79

Kisima chenye Hekima – Fred, C. N. W. Simiyu ........ 90

Mtu Mtandaoni – Sussy Nandama ........ 104

Pendo la Mhisani – Kitula King'ei ........ 113

Mchuuzi – Hanah Chaga Mwaliwa ........ 124

Funzo la Maisha – Mwenda Mbatiah ........ 135

Mke wa Mama – Rayya Timammy ........ 147

Kovu la Tuhuma – Evans Mbuthia ........ 159

Gharika ya Akili – Tom Olali ........ 170

Sumu ya Neno – Leo Sanja ........ 181

Nizikeni Mtandaoni – Fred, C. N. W. Simiyu ........ 195

Njiapanda –Fred Wanjala Wanyonyi .......................................207

Jeneza la Mama – Jeff Mandila........................................... 215

Lishe ya Sumu –Lilian Chacha ............................................223

Ndoto –Sharon A. Obanda ..................................................237

Daftari la Dadangu –Naomi Nzilani Musembi ................245

Barua ya Tatu –Titus Kaui ...................................................253

Digrii ya Majuto –Samson Ongarora Ontiri ....................265

Hadaa ya Ujana –Amiri Swaleh.......................................... 275

Mbona Hawaulizi? –K. W. Wamitila ................................284

Nani Angedhania–Sobongile Magwaza (imetafsiriwa na Kitula King'ei) .........................................................................297

Bakora ya Ulevi –Reuben, I. Kisiroche ...........................307

Bila Buriani –Deborah Nanyama Amukowa .................. 318

Simulizi za Manga –Beverlyne Asiko Ambuyo...............327

Shule ya Nyanya –Shadrack Amolloh............................. 337

Sherehe.......................................................................................348

Diwani ya *Kisima chenye Hekima na Hadithi Nyingine* inajumuisha maudhui mengi kuhusu mahusiano ya kijamii, elimu, uongozi, maarifa asili, ndoa, mazingira, utawala, TEHAMA, mihadarati na uvumbuzi wa maarifa miongoni mwa maudhui mengine ndani ya toni maridhawa. Mkusanyiko huu unaibua swali muhimu, je, jamii inastahili kufanya nini ili kujinasua? Tuna imani kwamba, hadithi zilizomo zitamsisimua na kumnasa msomaji kutokana na uketo wa ubunifu uliotumiwa katika diwani hii. Matumaini yetu ni kuwa, msomaji atavutiwa na hadithi hizi zenye mnato usio na kifani. Yaliyomo yana mchomo mkali wa kihisia, unaompa msomaji ilhamu ya kutaka kuchukua hatua. Mkusanyiko huu umejumuisha waandishi chipukizi na wale wenye uzoefu mkubwa. Muhimu hata hivyo ni kwamba, kuna uchu na ari ya kuibua masuala nyeti katika jamii na kuyaangazia kwa jicho pevu na kalamu yenye utelezi wa usimulizi na mbinu faridi za kughani. Tunawashukuru walimu na wanafunzi waliosoma baadhi ya hadithi hizi na kutoa maoni yao ambayo yalikuwa hazina kuu kwetu. Diwani hii inawalenga wanafunzi, wanachuo, wasomaji na wahakiki wote wa fasihi.

**Dkt. Fred, C. N. W. Simiyu - Chuo Kikuu cha Kibabii & Chuo Kikuu cha *the Free State***

**na**

**Leo Sanja Leonard - Chuo Kikuu cha Nairobi**

## Waandishi

K. W. Wamitila
Sanja Leo
Fred, C. N. W. Simiyu
Mwenda Mbatia Hanah
Chaga Mwaliwa Lilian
Zani
Naomi Nzilani Musembi
Beverlyne Asiko Ambuyo
Deborah Nanyama Amukowa
Aidah Mutenyo
Beatrice Luteshi
Kitula King'ei
Rayya Timmamy
Fred Wanjala Wanyonyi
Sharon A. Obanda
Titus Kaui
Sobongile Magwaza
Ernest Sangai Mohochi
Sussy Nandama
P. I. Iribemwangi
Tom Olali
Evans Mbuthia
Jeff Mandila
Purity Wangila
Samson Ongarora
Reuben, I. Kisiroche

TUNU PUBLISHERS
CHAKITA
ISBN 978-9966-59-027-5
9 789966 590275